# Jarida la UQAB

Toleo 8
Septemba 2017 Miladi
Dhul-Hijjah 1438 Hijriya

**Hotuba ya Mwanachuoni Mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Rashtah, Amir wa Hizb ut Tahrir kuhusu kuanza kwa mwezi wa Dhul Hijjah 1438 Hijria**

**Chanzo cha Mateso kwa Ummah Wetu**

**Nidhamu Ya Kiuchumi Ya Kirasilimali**

**Janga la Kiuchumi la Kiulimwengu**

**Starehe Fupi za Maisha ya Duniani**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 4**

**Maridhiano Kati ya Amerika na Ufaransa!**



## Maandamano ya Umwagikaji Damu Kenya: Ishara ya Kushindwa kwa Nidhamu ya Demokrasia



# Maandamano ya Umwagikaji Damu Kenya: Ishara ya Kushindwa kwa Nidhamu ya Demokrasia

Mnamo siku ya Ijumaa 11 Agosti 2017, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) ilimtangaza raisi aliye mamlakani Uhuru Kenyatta kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu wa 2017 uliofanywa mnamo Jumanne 8 Agosti. Bwana Kenyatta alijizolea kura 8,203,290 zikiwakilisha asilimia 54.27 ya kura zote zilizo pigwa. Mgombea uraisi wa muungano wa NASA Raila Odinga alikuwa wa pili kwa kura 6,762,224 zikiwakilisha asilimia 44.7 ya kura zote zilizo pigwa.

Tangazo hili lilikuja huku kukiwa na shutma kali kutoka kwa viongozi wa NASA wakisema kuwa uchaguzi huu haukuwa huru, wa haki na wazi. NASA ilidai kuwa mitambo (server) ya IEBC ilidukuliwa kuyageuza matokeo kumpendelea Kenyatta. Tume ya IEBC iliyapuuza madai hayo..

Hata kabla ya tangazo hili, ripoti za maandamano ya fujo zilikuwa zikiibuka nchini haswa katika maeneo ambayo ni ngome za kisiasa za Raila kama Kisumu, Homa Bay na Migori. Milio ya risasi ilisikika katika vitongoji duni vya Nairobi mnamo Ijumaa usiku baada ya raisi Uhuru Kenyatta kutangazwa mshindi. Katika kitongoji duni cha Mathare, waandamanaji wawili waliuwawa kwa kupigwa risasi ambapo polisi pia waliwarushia vitoa machozi watu walio choma magurudumu na kufunga barabara kwa siku nzima. Katika mji wa Kisumu, ulio watatu kwa ukubwa, waandamanaji kadhaa waliuwawa kwa kupigwa risasi.

Raisi mteule, Uhuru Kenyatta na mpinzani wake mkuu Raila Odinga – wote ni wanachama wa ngome mbili kuu za kisiasa zilizo pigania uongozi kwa miongo kadhaa tangu nchi hii ya Afrika Mashariki ilipopata 'uhuru' kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza mnamo 1964. Wanasiasa wote wawili ni vigogo wa kisiasa na wanafurahia ufuasi mkubwa sana kutoka kwa makabila yao. Huku ikitambuliwa kuwa kabila la Wakikuyu analotoka raisi Kenyatta ndilo kubwa zaidi nchini Kenya. Kabila la Wajaluo – la Raila Odinga ni la tatu kwa ukubwa nchini Kenya.

Kwa kutokea maandamano haya ya fujo, kuna hofu kuwa koloni hii ya zamani ya Uingereza huenda ikashuhudia kutokea tena kwa ghasia zinazohusishwa na chaguzi.

Siasa nchini Kenya zimenasibishwa na mivutano ya kikabila tangu wakati wa 'uhuru' mnamo 1963. Hii imeundwa na wakoloni wa Kiingereza walioitabanni na kuitumia kama mbinu ya kugawanya na kutawala katika uongozi. Kwa miaka, wamekuwa wakiichezea jamii moja dhidi ya nyengine, hususan Wakikuyu na Wajaluo ambao inawachukulia kuwa tishio kutokana na idadi yao kubwa. Vyama vikuu vya kwanza vya kisiasa kabla na baada ya uhuru wa Kenya – KANU na KADU – vilichochea siasa hizi za kikabila zilioko leo nchini. KANU ilikuwa chama cha muungano kati ya Wakikuyu na Wajaluo huku KADU ikijumuisha makabila mengine madogo yaliyo hofia kutawaliwa na KANU. KADU ilianzishwa na Daniel Arap Moi, Mkalenjin kutoka Bonde la Ufa.

Mnamo 1992, mji wa Molo ulikuwa ni kitovu cha ghasia za kikabila ambapo watu 5,000 walipoteza maisha yao. Mnamo 2007 jini la ukabila lilikuwa kubwa zaidi pindi baada ya kukataliwa matokeo ya kura za kitaifa lililo waacha zaidi ya watu 1,000 kufariki na maelfu wengine kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani. Hili lakini halipaswi kuchukuliwa kama somo tu la utafiti bali ni ishara ya kushindwa kwa nidhamu ya kisiasa ya demokrasia na wanasiasa wake ulimwengu mzima. Wanasiasa wa kidemokrasia wakiwemo wale wa nchi zinazoitwa 'zilizo komaa kidemokrasia' kama Amerika na Uingereza hutumia ukabila na ubaguzi wa rangi kufikia malengo ya kisiasa. Nchini Uingereza, jina la Enoch Powell si geni kwa hotuba yake ya kibaguzi maarufu kama hotuba ya Mito ya damu ya 1968. Yanayo shuhudiwa Kenya sasa hivi yamefichua sura halisi ya siasa za kidemokrasia – siasa za mgawanyiko zenye kuchochea ghasia na kuendelea kugawanya watu katika misingi ya kikabila, vyama na maeneo.

Ukitazama hali ya Kenya hususan ghasia zinazo husiana na uchaguzi yaweza kusemwa wazi wazi kuwa ajenda kuu ya chaguzi za kidemokrasia ni kushindania uongozi. Demokrasia ni kwa warasilimali wachache walio na uchu wa kujishibisha kibinafsi na hivyo basi wanasiasa hutumia njia yoyote chafu, kama kugawanya watu katika misingi ya kikabila, ili kuingia au kubakia uongozini. Urongo wa 'nchi zilizo komaa kidemokrasia' kuhusu demokrasia wapaswa kutofautishwa na sura halisi. Kusifu kwao demokrasia na chaguzi katika nchi yoyote ya ulimwengu wa tatu ni propaganda ya kimalengo kwa ajenda yao ya kiilmani ya kirasilimali. Chaguzi hizi ni pazia tu inayotumiwa kufinika kushindwa kwa warasilimali kutoweza kuwaunganisha watu na kuwasimamia mambo yao kikamilifu, na ni purukushani inayotumiwa kuwashughulisha watu kutofikia mageuzi msingi. Zaidi ya hayo, kura ni ala zinazo kusudiwa kuwafanya watumwa watu wa kawaida kutofanya kazi ya kuleta mageuzi ya kikamilifu, yaani, kuuleta Uislamu kama badala inayoweza kutatua matatizo yote ya mwanadamu na kuuangusha mfumo mbovu, wa kirongo na fisidifu wa kirasilimali.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Hotuba ya Mwanachuoni Mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Rashtah, Amir wa Hizb ut Tahrir kuhusu kuanza kwa mwezi wa Dhul Hijjah 1438 Hijria



وَالْفَجْرِ*وَلَيَالٍ عَشْرٍ

**“Naapa kwa al-Fajiri; na Masiku Kumi"** [Al-Fajr: 1-2]

(Imetafsiriwa)

Kwa wabebaji ulinganizi waaminifu, wasafi, wazuri na wema, ingawa hatumtakasi yeyote mbele ya Allah (swt).
Kwa wenye kuzuru tovuti waliojizatiti katika haki inayo tangazwa kwayo, na kheri inayo bebwa nayo kwa idhini ya Allah…

Kwa Waislamu wote wanaompenda Allah (swt) na Mtume wake (saw).

Kwa wote hawa, nawaamkua kwa maamkuzi ya Kiislamu, Assalamu Alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

Kama mujuavyo, imekuwa ada kwetu sisi kuwapongeza asubuhi ya siku ya Idd, lakini kwa kuwa imam amesoma katika swala ya al-Fajiri aya hii tukufu:

وَالْفَجْرِ*وَلَيَالٍ عَشْرٍ

**“Naapa kwa al-Fajiri; na Masiku Kumi"** [Al-Fajr: 1-2]

Nimeamua kuzungumza nanyi kuhusu masiku haya kumi tukufu ambayo Allah amechukua kiapo kwayo, na ambayo Mtume wa Allah (saw) imeifanya amali njema ndani yake kupendeza zaidi kwa Allah kuliko siku nyengine zozote. Amepokea Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Sa'eed bin Jubayr kutoka kwa Ibn Abbas aliye sema: Mtume wa Allah (saw) amesema:

ما من أيام العمل الصالح فيها أحب إلى الله من هذه الأيام - يعني أيام العشر - قالوا: يا رسول الله، ولا الجهاد في سبيل الله؟ قال: ولا الجهاد في سبيل الله، إلاّ رجل خرج بنفسه وماله ثم لم يرجع من ذلك بشيء

**“Hakuna siku ambazo amali njema ina pendeza zaidi mbele ya Allah kuliko siku hizi – yaani siku kumi za Dhul-Hijjah – (Maswahaba) wakamuuliza: Ewe Mtume wa Allah, hata kupigana Jihad katika njia ya Allah? (Mtume) akasema: Hata kupigana Jihad katika njia ya Allah, isipokuwa kwa mtu ambaye atatoka kwenda kupigana kwa nafsi yake na mali yake kisha kusirudi chochote katika hivyo (yaani afe shahidi).”**

Hizi ndizo siku bora kuanzia tarehe mosi ya mwezi mtukufu wa Dhul-Hijjah mpaka kumalizika kwa siku ya kuchinja ya Idd al-Adha, namuomba Allah Ta'ala kuujaalia kuwa na kheri na baraka kwa Uislamu na Waislamu. Na Allah azikubali ibada zetu, na kwamba masiku kumi haya yawe na kheri kwa yule atakaye yashuhudia kwa mema na kuyapa haki yake. Masiku haya ni masiku ya ukweli, ikhlasi na kujikaribisha kwa Allah kupitia amali njema na dua zenye kutakabaliwa kwa idhini ya Allah.

Kaka na Dada zangu:

Baadhi ya Mashabab wanasema kuwa usumbufu umezidi dhidi yetu kimataifa, kieneo na sehemu tunazoishi. Ndio hii ni kweli, lakini sio sababu ya kukata tamaa au kuhuzunika, bali ni kivuli cha faraja mbeleni, kwani ongezeko la janga huwa ni ishara ya faraja yake, na ongezeko la giza la usiku ni uashirio wa macheo ya kweli. Na hivi ndivyo ilivyo kuwa kwa makafiri wa Kiqureshi baada ya kuipiga vita Da'wah ya Mtume (saw) na kusimama dhidi yake (saw) kwa kila njia, huku wakiongeza na kuzidisha usumbufu wao. Wakamtenga Mtume (saw) na Maswahaba zake (ra), katika bonde na kuwatesa mpaka kusababisha miguu ya Mtume kumwagika damu. Wakamzulia

Endelea Uk..4

urongo Mtume (saw) wakimtuhumu uchawi, wazimu na urongo.

كَبُرَت كَلِمَةً تَخرُجُ مِن أَفوٰهِهِم ۚ إِن يَقولونَ إِلّا كَذِبًا

**"Ni neno kubwa hilo litokalo vinywani mwao* Hawasemi isipokuwa urongo tu."** [Al-Kahf: 5].

Hatimaye janga likaongezeka kwa kukubaliana kumuua Mtume wa Allah (saw). Wakamkimbiza (saw) mpaka katika pango la Thawr, ambamo yeye (saw) na Swahaba wake wa karibu Abubakar, Allah awe radhi naye, walijificha, na makafiri walisimama mlangoni mwa pango umbali wa dhiraa moja tu baina yao na Mtume (saw). Tukio hili lilitokea mkesha wa kuamkia siku ya hijra, na baada ya siku moja au mbili, Mtume (saw) akasimamisha serikali mjini Madina al-Munawwarah na kurefusha jengo lake ili kuang'aza Dini hii na kutangaza haki.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِأُولِي الْأَلْبَابِ

"Bila shaka katika hayo upo ukumbusho kwa wenye akili." [Az-Zumar: 21]

Na hivyo hivyo katika ulinganizi wetu tunaoubeba, kwa kufuata mfano wa Rasulullah (saw). Hizb ut Tahrir inayoongoza katika ulinganizi huu, mashabab wake na uongozi wake wamekabiliwa na kila aina ya usumbufu na mateso kufikia mpaka daraja ya kupata shahada, kutokana na njama za makhaini, dhulma za majasusi na uovu wa wenye chuki:

Ama kwa Hizb, imepigwa marufuku na kuzuiwa ndani ya nchi kadhaa za Ulimwengu wa Waislamu. Hata katika zile nchi zilizo ruhusu kuwepo na miundo ya vyama vya kila aina kama Indonesia, wameipiga marufuku harakati. Na nchi ambazo zimefungua milango kwa vyama vya kila aina, hata vilivyo potoka pia, kama Tunisia, wameipiga marufuku Hizb… Ama kuhusu ni kwa nini wamefanya hivyo? Jawabu ni kutokana na neno la haki ambalo Hizb inalitangaza.

Ama kwa Mashabab wa Hizb, jela za viongozi katili zinaelezea hadhi yao, kwani wamo ndani ya jela hizo za dhiki huku wakiteswa, na katika jela zao pana (nje) wanaandamwa. Kwa yakini, sisi tunatoka kwa Allah na kwake Yeye tutaregea.

Ama kwa uongozi wa harakati, Amiri wa kwanza alizuliwa urongo wazi wazi, na wenye chuki na majasusi, wakasema na kusema… Amiri wa pili hawakumzulia urongo tu, bali walidai kuwa alihujumu fikra na njia yake… ama mja dhaifu, Amiri wa tatu, hawakujifunga na uzushi pekee au kudai kuwa anahujumu fikra yake, bali walieneza uvumi wa kufariki kwake, wakidhani kuwa watapoza hasira zao! Hakika wao ni wajinga, kwa kuwa wana nyoyo lakini hawazingatii, kama kweli wanazingatia wangejua kuwa kifo cha Amiri wa Hizb hakimaanishi kufa kwa Hizb. Bali, Ata atapokezwa na mtu aliye na nguvu na imara zaidi atakaye wahutubia kwa maneno yake Ta'ala:

وَإِذَا خَلَوْا عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ ۚ قُلْ مُوتُوا بِغَيْظِكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

**"Na wanapokuwa peke yao wanakuumieni vidole kutokana na chuki. Sema: kufeni kwa chuki zenu! Hakika Allah anayajua yaliyomo vifuani"** [Ali-Imran: 119]

Da'wah hii mwenyewe ni Allah, na katu haitadhuriwa na njama za makhaini, dhulma za majasusi na uovu wa wenye chuki, na uzushi wa wazushi, bali itainuka juu juu zaidi na kueneza nuru yake mpaka mbinguni, kwa idhini ya Allah. Na ahadi ya Allah Ta'ala na bishara njema za Rasulullah (saw) zitatimizwa katika vigawanyo vyake vitatu:

Utawala huu wa kutenza nguvu utaanguka katika shimo na hatimaye Khilafah katika njia ya Utume itasimama. Mtume (saw) asema:

ثم تكون ملكًا جبرية فتكون ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها الله إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون خلافة على منهاج النبوة، ثم سكت

**"Kisha kutakuwepo na utawala wa utenzaji nguvu, utakuwepo kwa muda ambao Allah atataka uwepo kisha Allah atauondoa wakati anapotaka kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah katika njia ya Utume, Kisha akanyamaza".** (Imepokewa na Ahmad kutoka kwa Hudhayfah ibn al-Yaman) Ulimwengu utang'aa na Allah itaisimamisha haki na kuziondoa pango za makafiri…

Na tutaking'oa kidola cha kiyahudi. Muslim asema katika Sahih yake kutoka kwa riwaya ya Abu Hurayrah: Mtume (saw) asema:

لا تقوم الساعة حتى يقاتل المسلمون اليهود فيقتلهم المسلمون...

**"Hakitasimama Kiyama mpaka Waislamu wapigane na Mayahudi, na Waislamu watawaua…"** Katika riwaya nyengine, asema (saw):

يقاتلكم اليهود وتنصرون عليهم

**"Mayahudi watawapiga vita nyinyi na mutanusuriwa juu yao."**

Na tutaingia katika ardhi iliyo barikiwa tukiwa kama wakombozi, na kuswali katika Msikiti wa Al-Aqsa kwa adhan ya mwenzetu aliyeko Iraq, aliye tuma ujumbe ndani yake akiomba dua kwa Allah kumjaaliya kuwa Muadhini wa kwanza ndani ya Al-Aqsa baada ya kukombolewa kwake.

Pamoja na kuukomboa mji wa Roma, kwa idhini ya Allah. Amepokea Ahmad katika Musnad yake na Al-Haakim na kusahihishwa na Adh-Dhahabi kutoka katika riwaya ya Abu Qaabeel aliye sema:

**كنا عند عبد الله بن عمرو بن العاص، وسئل: أي المدينتين تفتح أولاً القسطنطينية أو رومية؟ فدعا عبد الله بصندوق له حلق، قال: فأخرج منه كتاباً، قال: فقال عبد الله: بينما نحن حول رسول الله صلى الله عليه وسلم نكتب إذ سئل رسول الله صلى الله عليه وسلم: أي المدينتين تفتح أولاً قسطنطينية أو رومية؟ فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم: مدينة هرقل تفتح أولاً يعني قسطنطينية.**

**"Tulikuwa na'Abdullaah ibn 'Amr ibn al-'Aas ilipo ulizwa ni mji gani utakao fungliwa mwanzo, Kostantiniyya (leo Istanbul) au Roma? 'Abdullaah akasema, "Tulipo kuwa pambizoni mwa Mtume (saw) tunaandika, aliulizwa Mtume (saw): kati ya Miji miwili, ni upi utakao funguliwa mwanzo Kostantiniyya au Roma? Mtume (saw) akajibu: Mji wa mfalme Kisra**

*Endelea Uk..5*

**yaani Kostantiniyya."**

Kostantiniya ushafunguliwa bado kufunguliwa Roma, InshaAllah, na matarajio ya mwenzetu wa Falastin aliye tuma barua akiomba dua kwa Allah kumruzuku kipande cha ardhi ndani ya mabonde ya Roma kama mfano wa Tamim al-Dari, Allah awe radhi naye, yatatimia.

Hivyo basi, hakutakuwa na nyumba yoyote iliyo jengwa kwa udongo wala sufi ambayo utukufu wa mwenye nguvu au idhlali ya mwenye kudhalilika haitaingia ndani yake. Utukufu ambao Allah ataupatia Uislamu, na idhlali ambayo (swt) ataipatia ukafiri.

Amesema Mtume (saw) katika hadith iliyo pokewa katika Musnab ya Ahmad kutoka kwa riwaya ya Tamim al-Dari asema: Nimemsikia Mtume wa Allah (saw) akisema:

**"ليبلغن هذا الأمر ما بلغ الليل و النهار ، و لا يترك الله بيت مدر و لا وبر إلا أدخله الله هذا الدين بعز عزيز أو بذل ذليل عزا يعز الله به الإسلام و ذلا يذل به الكفر " .**

"Allah atalifikisha jambo hili (Uislamu) kila panapo fikiwa na usiku na mchana, wala hataiwacha hata nyumba moja iliyo jengwa kwa udongo wala kwa sufi isipokuwa ataiingiza ndani yake dini hii kwa izza ya mwenye izza na idhlali ya wenye kudhalilika, Allah ataupa izza Uislamu na kuudhalilisha ukafiri…" Baihaqi amepokea hadith sawa na hii katika As-Sunan Al-Kubra pia katika Mustadrak ya Hakim.
Waovu na wazushi, wale ambao nyoyo zao zina maradhi ya ufisadi katika ardhi, watasema kuwa tunaota, au ni waotaji… wanaofanana nao washatangulia kusema haya. Walisema kuhusu Mtume wa Allah (saw), na Maswahaba zake, Allah awe radhi nao: dini yao imewadanganya, wataweza vipi kuzifikia hazina za Kisra na Kaisari?! Hatimaye ahadi ya Allah ikatimia licha ya uovu wa wale walio angamia. Kwa hivyo, Kisra na Kaisari walianguka na dola ya Kiislamu na bendera yake ikasimama, hili pia litajirudia tena kwa idhini ya Allah, na wenye chuki watakufa na chuki zao na kufuatiwa na dhulma za majasusi na makhaini na kila anaye zungumza batili.

**وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنقَلَبٍ يَنقَلِبُونَ**
"Na ndipo watakapo jua wale wanao dhulumu ni mgeuko gani watakao geuka."
[Ash-Shu'ara: 227].

Kaka na Dada zangu:

Hatufanyi kazi tu kwa ajili ya kujipumbaza, bali tunafanya kazi tukiwa na imani na ahadi ya Allah, ambayo sio tu kwa Mitume, na sio ya Akhera pekee, bali pia ni kwa Waumini hapa duniani na kesho Akhera.

**إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ**
Hakika sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watakapo simama Mashahidi (kutoa ushahidi wao) ..." [Ghafir: 51].
Nawaahidi kaka na dada zangu, kwamba Hizb tangu kubuniwa kwake mpaka leo, mara nyingi imekaribia kufikia malengo yake, lakini

**لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ**
"Kila kipindi kina hukmu yake." [Ar-Ra'd: 38].

Na Allah ndiye aliye na hikma pana… ikiwa Al-Qaweey Al-Aziz amepitisha jambo, hulipatia sababu nyepesi za kulifikia na wala halita cheleweshwa

**إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ ۚ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا**
**"Hakika Allah atatimiza amri yake. Hakika Allah amejaalia kila kitu na kipimo chake."** [At-Talaq: 3].

Kutamatisha, narudia tena yale niliyo anza nayo, nazungumza nanyi katika siku ya mwanzo ya siku hizi kumi zilizo barikiwa, ambazo Allah aliapa kwazo, na Mtume wa Allah (saw) kuzungumza kuzihusu:

**ما من أيام العمل الصالح فيها أحب إلى الله من هذه الأيام - يعني أيام العشر (من ذي الحجة)**

"Hakuna siku ambazo amali njema ina pendeza zaidi mbele ya Allah kuliko siku hizi – yaani siku kumi za Dhul-Hijjah".

Hizi ni siku bora, kuanzia tarehe mosi ya mwezi mtukufu wa Dhul-Hijjah mpaka kumalizika kwa siku ya kuchinja ya Idd al-Adha, namuomba Allah Ta'ala kuujaalia kuwa na kheri na baraka kwa Uislamu na Waislamu. Na Allah azikubali ibada zetu, na kwamba masiku kumi haya yawe na kheri kwa yule atakaye yashuhudia kwa mema na kuyapa haki yake. Masiku haya ni masiku ya ukweli, ikhlasi na kujikaribisha kwa Allah kupitia amali njema na dua zenye kutakabaliwa kwa idhini ya Allah… Namuomba Allah azirudishe tena siku zile tuwe chini ya kivuli cha bendera ya Uqab tumiliki kheri kubwa mikononi mwetu, na ndimi zetu kuitamka, nyoyo zitulizane, na vifua kupanuka kwa ajili yake:

**وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ* بِنَصْرِ اللَّهِ ۚ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۖ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ**
**"Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusra ya Allah, humnusuru amtakaye na ndiye mwenye nguvu mwenye kurehemu."** [Ar-Rum: 4-5].
Kutamatisha pia, nakariri tena kuwa Da'wah hii mwenyewe ni Allah, na kamwe haitadhuriwa na njama za makhaini, dhulma za majasusi, au uovu wa wenye chuki, wala uzushi wa wazushi, bali ulinganizi wa Allah utainuka, na nuru yake itawavutia watazamaji mukhlisina na muangaza wake utaziweka mbali nyoyo za wenye chuki na hasadi.

**وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ**
**"Na bila ya shaka mutajua habari zake baada ya muda."** [Sad: 88]

Wassalamu Alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

Ndugu Yenu,

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**Amir wa Hizb ut Tahrir**

**1 Dhul Hijjah 1438 H**
**23/08/2017 M**

# Tusiwache Kuhangaika Kwetu Kujitafutia Utajiri Kuwe ni Chanzo cha Mateso kwa Ummah Wetu




Katika wakati ambapo maadui wa Waislamu wameongeza uadui wao, na Waislamu, kuanzia Masjid al-Aqsa na Syria, mpaka eneo lililokaliwa la Kashmir na Afghanistan, wameongeza kuasi kwao kiungwana, kila afisa wa majeshi yetu ni lazima sasa ajitathmini kwa kina. Ni lazima akubali kuwa kizuizi cha muamko wa Ummah hakiko kwengine ila kwake kwani yeye ni miongoni mwa watu wanaomiliki nusra, nguvu na ulinzi.

Yeye, na wengine kama yeye, ndio wenye uwezo wa kuondoa kizingiti kilichoko sasa, kuutoa Ummah kutoka katika idhilali mbele ya maadui zake, hadi kuwatawala juu yao. Kwa hivyo, ni lazima atafakari ni kitu gani kilichomzuia kusonga mbele kabla na sasa. Huku akifanya hivyo, ni lazima awe na hisia sahihi ya mazingira yaliyo undwa ndani ya jeshi leo kuzuia harakati ya mageuzi na uhuru wa kikweli. Ni lazima atafute muongozo kutoka katika dini ili asibakie kuwa mtazamaji tu wa mgongano baina ya Ummah na wakoloni wavamizi. Hapo ndipo afisa huyu wa jeshi atakapo jitokeza kama mlinzi muaminifu anaye tafuta ushindi mkubwa kwa Ummah.

Afisa huyu anapaswa kulichukulia joto lililoko sasa na mazingira yanayo zuia kupiga hatua, kuwa si yenye kutokea kibahati mbaya tu. Kutokana na utawala wa kiulimwengu wa mfumo wa kimada wa kirasilimali, kuhangaika kutafuta utajiri wa kimada imekuwa ndio lengo msingi maishani. Kutokana na maslahi duni ya kimada, urafiki huundwa na kuvunjwa, mafungamano hudumishwa na kukatwa, majukumu hutekelezwa na kupuuzwa. Kwa kukosekana Uislamu kama mfumo kamili wa maisha, utajiri umekuwa ndio kipimo cha mafanikio na hadhi katika jamii. Kuhangaika kwa ajili ya kupata utajiri mkubwa imekuwa ndio jambo kubwa linalo washughulisha, miongoni mwa wenye msemo kwa jumla, na wanajeshi haswa.

Katika kadhia ya Pakistan, inayo miliki jeshi kubwa na lenye nguvu zaidi katika ulimwengu wa Waislamu, tunaona katika vilabu vya gofu na vilabu maalumu mila ya kushindana juu ya mapato ya kidunia. Mazungumzo yametawaliwa na ulinganishaji wa majumba, magari, taasisi za elimu kwa watoto, harusi zilizo pita mipaka, uwekezaji wa kibiashara na kiwango cha uwekaji akiba pesa. Katika mafunzo ya kijeshi ya kigeni, pamoja na miundo yote ya kimawasiliano ya kigeni, wamagharibi wako makini kuhisi na kukuza kasumba ya kimada ndani ya kila afisa, kwani huu ndio ufunguo wa kuwadhibiti. Hivyo basi si ajabu kuwa wengi katika wanajeshi, hususan katika ngazi za juu, wamekusanya utajiri wa kutosha kwa maisha yao yote na hiki kimekuwa ndio kipimo kwa wale walio chini yao. Nyaraka za Panama na kesi za taasisi ya kitaifa ya kuwahisabu walio na mamlaka zinatoa mtazamo wa ukusanyaji mkubwa wa utajiri miongoni mwa watu wenye msemo na walio bahatika. Huku utajiri huu ukidaiwa na wengine kuwa wenye kupatikana kiharamu, na wengine, kuwa wa halali, hakuna hata mmoja anaye weza kukataa kuwa viwango hivi vikubwa ndivyo vilivyo sababisha kuwepo na mazingira ya ufisadi.

*Endelea Uk..7*

Tunapo tazama zama bora za Ummah wetu, zama za Khilafah na Jihad, tutaona dhihirisho la hali yetu ya sasa. Tuliweza vipi wakati huo kuonja ushindi na nguvu juu ya maadui zetu kwa makarne, na sasa hivi tunashindwa? Kisha, mashindano miongoni mwa majeshi yetu yalikuwa juu ya ufunguzi wa ardhi mpya kwa Uislamu na kuikumbatia shahada. Ummah uliweza kupata ushindi juu ya maadui zake, licha ya idadi yao kubwa ya majeshi na silaha. Kitambo Waislamu waliuchukulia utajiri kuwa kifaa, huku lengo la maisha na kipimo cha mafanikio vikiwa ni kutawala kwa dini yetu. Mpaka hapa, afisa wa jeshi na azingatie kuwa katika utangulizi wa katiba, kama ilivyo tayarishwa na Hizb ut Tahrir kwa Khilafah inayo kuja, elimu ya kijeshi itakuwa na sehemu nzito ya Uislamu.

Kama Hizb ut Tahrir ilivyo tabanni katika kifungu cha 67, "Ni wajib kulipatia jeshi kiwango cha juu zaidi cha elimu ya kijeshi ili kuinua kiwango chao cha kifikra kwa kadri inavyo wezekana. Kila mwanajeshi anapaswa kupewa thaqafa ya Kiislamu itakayo muwezesha kuwa na utambuzi wa Uislamu, angaa kwa kiwango jumla." Leo, Waislamu walio maafisa wa jeshi ni lazima wajitazame ndani yao, kwa kutumia dini yetu kama kipimo, kupambana dhidi ya maslahi na matamanio ya vyeo vyao, ili kujitokeza kuunusuru Ummah katika wakati huu unapo wahitajia mno.
Kwa wanaume wanaotaka kuvunja kizingiti hiki, na wazingatie kwa makini hikma iliyopo katika maonyo ya Mtume wa Allah (saw) kuhusiana na tamaa ya utajiri iliyo pitiliza mipaka. Ka'ab bin 'Iyad anahadithia kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) akisema:

«إِنَّ لِكُلِّ أُمَّةٍ فِتْنَةً وَفِتْنَةُ أُمَّتِي الْمَالُ»

**"Hakika katika kila Ummah kuna fitna na fitna ya Ummah wangu ni mali"** [Tirmidhi].

Ibn Ka'ab bin Malik Al-Ansari anahadithia kutoka kwa babake, kuwa Mtume wa Allah (saw) amesema:

«مَا ذِئْبَانِ جَائِعَانِ أُرْسِلاَ فِي غَنَمٍ بِأَفْسَدَ لَهَا مِنْ حِرْصِ الْمَرْءِ عَلَى الْمَالِ وَالشَّرَفِ لِدِينِهِ»

**"Mbwa mwitu wawili walio miongoni mwa kondoo si waharibifu kwao kushinda mtu aliye na tamaa ya mali na cheo kuliko dini yake."** [Tirmidhi].

Ni vipi basi mtu anaye shuhudia uharibifu huu wa Ummah mbele ya macho yake na fitna juu ya fitna, atanyamazia kimya kutokana tu na kiu ya utajiri? Ikiwa atabakia kufungika katika minyororo ya uchu wa kujitajirisha binafsi, anajinyima fursa ya kutukuzwa milele na milele kesho Akhera kwa kuinusuru dini yetu!

Na wazingatie kuwa uchu wa kupata utajiri ni katika umbile la mwanadamu, ghariza (hisia) yake ya kuhifadhi maisha iko juu. Kihakika, kama tunavyo taka kujihifadhi dhidi ya kitu chengine chochote, tusidharau pia matamanio. Wala tusidharau pia maafa yake ambayo yaweza kusababisha juu ya majukumu ya mja anaye taka radhi za Allah (swt), kama kipaumbele cha maisha yake. Anas b. Malik amepokea katika hadith ya Mtume wa Allah (saw) akisema:

«لَوْ كَانَ لِابْنِ آدَمَ وَادٍ مِنْ ذَهَبٍ أَحَبَّ أَنَّ لَهُ وَادِيًا آخَرَ وَلَنْ يَمْلأَ فَاهُ إِلاَّ التُّرَابُ وَاللَّهُ يَتُوبُ عَلَى مَنْ تَابَ»

**"Lau Mwanadamu angekuwa na bonde la dhahabu angependa awe na bonde la pili na hakuna kitakacho jaza mdomo wake isipokuwa mchanga na Allah humsamehe mwenye kutubia"** [Muslim].

Zaidi ya hayo, hamu ya kutaka utajiri iko juu hata kwa mtu aliye zeeka na kupanda ngazi za juu katika taasisi ya kijeshi, ingawa mauti ni jambo la kawaida. Anas bin Malik amehadithia kutoka kwa Mtume (saw) akisema:

«يَهْرَمُ ابْنُ آدَمَ وَيَشِبُّ مِنْهُ اثْنَتَانِ الْحِرْصُ عَلَى الْعُمُرِ وَالْحِرْصُ عَلَى الْمَالِ»

**"Mwanadamu anazeeka lakini vitu viwili havizeeki kwake: tamaa ya umri na tamaa ya mali"** [Tirmidhi]

Uislamu, kama ulivyo teremshwa na Muumba (swt) wa mwanadamu pamoja na utajiri, uliitibu hamu hii katika njia bora zaidi. Lau tutajifunza, kutafakari na kubadilika, hatutafungwa na minyororo ya maisha haya mafupi ya dunia, na kuyatupa maisha yetu ya milele ya Akhera.

Kwa hivyo, Uislamu umetukumbusha kuwa utajiri wa kihakika unao tunufaisha sio ule tulio ukusanya na kuwaachia warithi wetu, bali ni ule uliotumiwa kwa ajili ya Allah (swt). Mutarrif amepokea kutoka kwa babake: Nilikuja kwa Mtume wa Allah (swt) alipo kuwa akisoma:

(أَلْهَاكُمُ التَّكَاثُرُ)

**"Utawashughulisheni nyinyi ukusanyaji mali"**[Surah at-Takaathur 102:1].
Akasema: «يَقُولُ ابْنُ آدَمَ مَالِي مَالِي»
"Anasema mwanadamu: mali yangu, mali yangu". Na yeye (saw) akasema:

«وَهَلْ لَكَ يَا ابْنَ آدَمَ مِنْ مَالِكَ إِلاَّ مَا أَكَلْتَ فَأَفْنَيْتَ أَوْ لَبِسْتَ فَأَبْلَيْتَ أَوْ تَصَدَّقْتَ فَأَمْضَيْتَ»

**"Je, ewe mwanadamu, una mali yoyote isipokuwa ile ulio kula ikamalizika au ulio vaa ikachakaa au ulio toa sadaqa ukaitanguliza mbele?"** [Muslim].

Katika hadith sawa na hii, Abu Huraira (ra) amepokea kutoka kwa Mtume (saw) akisema:

«يَقُولُ الْعَبْدُ مَالِي مَالِي إِنَّمَا لَهُ مِنْ مَالِهِ ثَلاَثٌ مَا أَكَلَ فَأَفْنَى أَوْ لَبِسَ فَأَبْلَى أَوْ أَعْطَى فَاقْتَنَى وَمَا سِوَى ذَلِكَ فَهُوَ ذَاهِبٌ وَتَارِكُهُ لِلنَّاسِ»

**"Mja anasema: mali yangu mali yangu, hakika mali yake ni katika mambo matatu tu; alicho kula kikamalizika au alicho vaa kikachakaa au alichotoa akakiweka (kesho akhera) yasiyo kuwa haya ataondoka na kuwaachia watu"** [Muslim].
Anas bin Malik (ra) anahadithia kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) akisema:

يَتْبَعُ الْمَيِّتَ ثَلاَثَةٌ، فَيَرْجِعُ اثْنَانِ وَيَبْقَى مَعَهُ وَاحِدٌ: يَتْبَعُهُ أَهْلُهُ وَمَالُهُ وَعَمَلُهُ، فَيَرْجِعُ أَهْلُهُ وَمَالُهُ، وَيَبْقَى عَمَلُه

**"Vitu vitatu vinamfuata maiti,**

*Endelea Uk..8*

**viwili vinarudi kimoja kinabakia naye: wanamfuata watu wake, mali yake na amali yake. Watu wake na mali yake vina rudi, amali yake inabakia.”** [Bukhari].

Maafisa wa ngazi za juu zaidi jeshini na wazingatie kuwe lau watakufa kesho, ni wachache watakaosema kuwa walikufa wakiwa wadogo. Na wajiulize maswali, ni vipi basi kuhusu utajiri ambao kwao walitafuta raha na utilivu? Utajiri huo utamnufaisha nani, isipokuwa warathi wao? Utajiri huo hautakuwa na manufaa kwao, huku wakimkabili Allah (swt) kuulizwa maswali kuhusiana na uwezo wao waliokuwa nao na waliufanyia nini katika zama hizi za idhlali? Na wazingatie basi maneno ya Allah (swt) alipo sema:

يَوْمَ لا يَنْفَعُ مَالٌ وَلا بَنُونَ * إِلاَّ مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

**“Siku ambayo haitanufaisha mali wala watoto - Isipokuwa (atanufaika) yule atakayemjia Allah na moyo uliosalimika”** [Surah ash-Shura’a 26:88-89]

Maafisa na wazingatie kuwa hamu ya utajiri haipaswi kuishinda ari ya kujitolea katika matendo mema wakati wowote, haswa wakati ambapo matendo mema hayo yana uwezo wa kuleta wimbi la mageuzi kwa Ummah huu kipenzi. Allah (swt) asema:

الْمَالُ وَالْبَنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَالْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ عِندَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَخَيْرٌ أَمَلًا

**“Mali na watoto ni mapambo ya maisha ya dunia. Lakini yaliobakia katika mema ni thawabu bora mbele ya Mola wako na matarajio mema”** [Surah Al-Kahf 18:46]
Ibn ‘Abbas (ra) asema:

هي ذكر الله ، قول : لا إله إلا الله ، والله أكبر ، وسبحان الله ، والحمد لله ، وتبارك الله ، ولا حول ولا قوة إلا بالله ، وأستغفر الله ، وصلى الله على رسول الله ، والصيام ، والصلاة ، والحج ، والصدقة ، والعتق ، والجهاد ، والصلة ، وجميع أعمال الحسنات. وهن الباقيات الصالحات ، التي تبقى لأهلها في الجنة ، ما دامت السموات والأرض

**“Kumkumbuka Allah ni katika maneno: ‘La ilaha illallah, Allahu Akbar, Subhan Allah, Al-Hamdu Lillah, Tabarak Allah, La hawla wa la quwwata illa billah, Astaghfirallah, Sallallahu ‘ala Rasul-Allah’, na saumu, swala, hajj, sadaqah, kuacha huru mtumwa, Jihad, kuunganisha kizazi, na amali zote nyengine njema. Hizi ndizo amali zitakazo bakia kwa watendaji wake peponi, kwa wale watakao zifanya maadamu mbingu na ardhi zitabakia kuwepo kwake”**

Allah (swt) pia ameonya:

وَاعْلَمُواْ أَنَّمَآ أَمْوَٰلُكُمْ وَأَوْلَـٰدُكُمْ فِتْنَةٌ وَأَنَّ اللَّهَ عِندَهُۥٓ أَجْرٌ عَظِيمٌ

“Na jueni kuwa hakika mali zenu na watoto wenu ni fitna na mbele ya Allah kuna malipo makubwa.” [Surah Anfaal 8:28]
Na Allah (swt) ameonya:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ لاَ تُلْهِكُمْ أَمْوَٰلُكُمْ وَلاَ أَوْلَـٰدُكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ فَأُوْلَـٰئِكَ هُمُ الْخَـٰسِرُونَ

**“Enyi Mulioamini! Zisiwashughulisheni mali zenu wala watoto wenu katika kumkumbuka Allah. Na atakaye fanya hivyo ni katika walio hasirika.”** [Surah Munafiqun 63:9]
Afisa wa jeshi anayetaka kufuata njia ya Maanswari (ra), waliotoa nusra kwa Uislamu hapo awali, aufunge moyoni wake barabara kuwa mafanikio na cheo cha kihakika hayapatikani kupitia utajiri. Abu Huraira (ra) amepokea kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) akisema:

إِنَّ اللَّهَ لاَ يَنْظُرُ إِلَى صُوَرِكُمْ وَأَمْوَالِكُمْ وَلَكِنْ يَنْظُرُ» «إِلَى قُلُوبِكُمْ وَأَعْمَالِكُمْ

**“Hakika Allah haangalii sura zenu na mali zenu lakini ana angalia nyoyo zenu na amali zenu.” [Muslim]**
Imepokewa kutoka kwa Samurah bin Jundab kwamba Mtume wa Allah (saw) asema:

«الْحَسَبُ الْمَالُ وَالْكَرَمُ التَّقْوَى»

**“Heshima ni mali na ukarimu ni ucha Mungu.”** [Ibn Maajah].

Na ajitakase kutokana na athari fisidifu na kusimama kama mkombozi wa Ummah huu. Na ajitokeze sasa, bila ya kusitasita, akitafuta cheo sawa na cha nduguye wa kijeshi aliye mtangulia katika kutoa nusra kusimamisha Uislamu kama serikali na utawala, naye ni Sa’ad ibn Muadh (ra). Pindi Sa’ad (ra) alipo fariki, mamake alilia na Mtume wa Allah (saw) akamwambia:

ليرقأ (لينقطع) دمعك، ويذهب حزنك، فإن ابنك أول›› ››من ضحك الله له واهتز له العرش

**“Machozi yako yatasita, na huzuni yako itatoweke,utakapojua hakika mwanao ndiye mtu wa kwanza kumfanya Allah acheke na Arshi yake itingishike.”** [At-Tabarani].

Afisa wa jeshi wa zama hizi na ajitolee nafsi yake na mali yake kwa ajili ya Allah (swt) kwa lengo la kupata Jannah katika biashara bora ambayo yapaswa kuonewa wivu! Allah (swt) asema:

إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُم بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ ۚ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ ۖ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنجِيلِ وَالْقُرْآنِ ۚ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ ۚ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُم بِهِ ۚ وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**“Hakika Allah amenunua kutoka kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa badali ya pepo* Wanapigana katika njia ya Allah; wanauwa na kuuwawa. Ahadi yake ni ya kweli katika Taurati na Injili na Quran. Na ni nani mkweli zaidi katika utekelezaji ahadi asiye kuwa Allah? Basi pokeeni bishara njema ya biashara yenu mulio ifanya. Na huko ndiko kufaulu kukubwa.”** [Surah At-Tawba 9:111]

**Musab Umair**
**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Athari fisidifu za muundo wa Nidhamu ya Kiuchumi ya Kirasilimali




Ni ukweli usiopingika kuwa jengo lolote linapojengwa juu ya msingi fisidifu huwa jengo hatari kwa usalama na wakati wowote huweza kuporomoka. Asema Allah (swt):

أَفَمَنْ أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ تَقْوَىٰ مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٍ خَيْرٌ أَمْ مَنْ أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ شَفَا جُرُفٍ هَارٍ فَانْهَارَ بِهِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**Je, mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya kumcha Allah na radhi zake ni bora au mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo linalo poromoka lika poromoka naye katika moto wa Jahanam? Na Allah hawaongozi watu madhalimu.** [At-Tawbah: 109]

Uhakika huu ndio unaojitokeza leo katika muundo wa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali uliojengwa juu ya Aqeeda fisidifu ya kiilmani inayo mpokonya Muumba haki ya kuendesha maisha ya waja wake na badala yake kuwapa waja wenye akili finyo, na mwenye sifa ya ubinafsi, mamlaka hayo. Natija yake tunashahudia kusheheni dhulma na matatizo yanayosababisha dhiki na mateso kwa wanadamu katika kila nyanja ya maisha yao ikiwemo uchumi.

Jengo la uchumi wa kirasilimali limesimama juu ya nguzo tatu:
1) Nidhamu ya Fedha na Mabenki
2) Makampuni ya Kirasilimali
3) Sarafu ya Karatasi

Katika Toleo hii la UQAB tutajifunga na nguzo ya kwanza kwa kuonyesha athari zake mbaya ilizoleta kwa wanadamu.

**Nidhamu ya Fedha na Mabenki**

Taasisi za kifedha na mabenki ya kirasilimali zimebuniwa juu ya msingi fisidifu ambao ni kujipatia thamani ya kimada ili kushibisha mahitajio kwa wawekezaji pasi na kuzingatia uharibifu utakaosababishwa na lengo hilo kwa mtu binafsi au jamii nzima.

Kwa mujibu wa kipimo chetu cha kiislamu, mfumo wa fedha na mabenki wa kirasilimali umejengwa juu ya msingi wa mambo mawili batil:

a) Riba, ambayo Allah (swt) ametutahadharisha nayo akisema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبَا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ* فَإِنْ لَمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ...

**Enyi Mulio amini mcheni Allah na acheni katika riba iliyo bakia ikiwa nyinyi ni Waumini wa kweli* Basi ikiwa hamutafanya hivyo jitangazieni vita na Allah na Mtume wake…**[Al-Baqarah: 278-279]

b) Ulimbikizaji mali (Kanz) ambayo pia Allah (swt) ametuonya kwa ukali akisema:

وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

**na wale wanao limbikiza dhahabu na fedha wala hawazitumii katika njia ya Allah wabashirieni adhabu kali** [At-Tawbah: 34]

Taasisi hizi aghalabu hubuniwa kupitia makampuni ya kibinafsi, yanayomilikiwa na mabwenyenye, au kundi la mabwenyenye, au hubuniwa kupitia mpangilio wa hisa.

Utendakazi wa taasisi hizi hujitokeza katika sura tatu zifuatazo:

**Kwanza:** utumizi wa mali iliyo kusanywa kutoka kwa watu tofauti tofauti kutoka kwa wamiliki wa akaunti kwa kiwango kidogo cha riba, hatimaye kukopesha wengine kwa kiwango kikubwa cha riba.
**Pili:** ni kwa kupitia taasisi hizi kuweka pesa zake kwa taasisi nyengine kuu za kifedha ndani ya nchi au nje ya nchi ili kuvuna kiwango kikubwa zaidi cha riba.
**Tatu:** kuanzisha miradi mbali mbali ambayo ufadhili wake huweza kufanyika kupitia kuzifunga baadhi ya akaunti za wateja kwa muda mrefu. Manufaa badali yake ni kwa wateja hawa ni kupewa nyongeza ya riba kwa pesa zao.

*Endelea Uk..10*

**Athari zake Fisidifu**

Athari za taasisi hizi ni nyingi mno kushinda kifani. Athari mbili zifuatazo ni miongoni mwa athari kuu mbaya za taasisi hizi:

**1) Mzunguko wa Pesa**
Mzunguko wa pesa umefungika katika mikono ya wachache katika jamii. Yaani kupitia riba, pesa huchukuliwa kutoka mikononi mwa watu na kupitia riba vile vile, mabwenyenye wakubwa wa kirasilimali walio na uwezo wa kuwekeza na kulipa mikopo, huchukua viwango vikubwa vya pesa kutoka mabenki haya. Natija yake, husababisha masikini kuzidi kuwa masikini na matajiri huzidi kutajirika kwa kujipanua kibiashara. Hatimaye mabwenyenye hawa huanzisha miradi mikubwa inayoutawala uchumi wa nchi na hivyo basi kuwafanya masikini kuishi chini ya huruma ya tabaka hili kwa kutegemea bidhaa na huduma wanazozalisha kwa bei wanayoitaka wao (matajiri).

Hivyo basi uwekaji pesa benki kwa watu wa kawaida ndio unaotoa mwanya kusababisha maafa haya kwao, kinyume na vile walivyo amini kuwa itawaletea wao faida; na hiyo faida ya riba wanayopewa na benki ndio mkondo wa maji unaojaza bahari ya matajiri.

**Suluhisho**

Katika serikali ya Khilafah kamwe hakutoruhusiwa kuweko na taasisi hizi zilizojengwa juu ya msingi wa mambo hayo miwili tulioyataja ambayo yanakhalifu sharia ya Kiislamu. Kwa kuwa huu ndio msingi wa mabenki haya, kutoweka kwake itakuwa jambo lisilokuwa na budi.

Khilafah itatatua janga hili kivitendo kupitia njia zifuatazo:

a. Kulea Ummah wenye Shakhsiya ya Kiislamu wanaopenda na kuchukia kwa ajili ya Allah (swt) katika mtaala wa elimu ya mashule na vyuo.
b. Kutoa mikopo isiyokuwa na riba au ruzuku kutoka katika diwani ya ruzuku (ديوان العطاء) hivyo basi kushurutisha matajiri binafsi kufuata mwenendo.
c. Kukataza ulimbikiza mali kupitia kwa mfano kubuni chombo cha ushirikiano na muungano wa kibiashara (CBPA) katika diwani ya maslahi ya dola (ديوان مصالح الدولة) kitakachohamasisha na kusimamia ushirika wa kibiashara kati ya wenye mali ziada na wajuzi wa fani mbali mbali ikiwemo serikali yenyewe.
d. Serikali kufungua matawi ya Bait ul-Maal katika kila Wilayah na Imalah ili kurahisisha shughuli za kifedha baina yake na raia au baina ya raia wao kwa wao.
e. kuweka adhabu kali kwa atakaye jihusisha na riba au ulimbikizaji wa mali.

**2) Ugurishaji wa Mali Kutoka Nchini Kwenda Nje**

Kupitia taasisi hizi pia mali hugurishwa kutoka katika nchi masikini au zilizo katika 'Ulimwengu wa Tatu' kwenda katika nchi zilizo 'Endelea'. Hii ni kupitia njia mbili zifuatazo:

i. Kwanza: Kupitia kuasisiwa kwa mabenki ya kigeni nchini na hivyo basi kuchukuliwa pesa moja kwa moja kutoka mikononi mwa wananchi kwa manufaa ya serikali za kigeni.

ii. Pili: pesa pia hugurishwa kupitia benki za humu nchini kuchukuwa pesa mikononi mwa wananchi kwa kiwango kidogo cha riba takriban asilimia 7 au 8, na hatimaye kuziwekeza katika mabenki ya kimagharibi ng'ambo kwa lengo la kuvuna kiwango kikubwa cha riba ambacho hufikia mabilioni ya dola.

Hii ni hatari kubwa kwa nchi, kwa kule kuinyima rasilimali ambayo ingeiwezesha kuanzisha miradi tofauti tofauti, badala yake imeiweka nchi mikononi mwa nchi za mabepari kwa kuwanufaisha katika miradi yao.

Mfano wa nchi za Waislamu zilizo salimisha rasilimali zake mikononi mwa nchi za mabepari kulingana na takwimu za mwaka wa 2013: (Miongoni mwa Nchi 50 za Juu imejumuisha: Na.34 UAE; $61,960,000,000, Na.35 Kuwait; $60,760,000,000, Na.41 Turkey; $33,440,000,000 Na.42 Qatar; $28,860,000,000, Na.43 Kazakhstan; $26,530,000,000, Na.44 Saudi Arabia; $26,080,000,000, Na.46 Tajikistan $18,500,000,000, Na.47 Libya; $17,820,000, Na.48 Indonesia $17,410,000,000,). https://en.wikipedia.org/wiki/List_of_countries_by_FDI_abroad
Idadi ya rasilimali jumla yote iliyoko ng'ambo ni zaidi ya dola bilioni 291.

**Suluhisho**

Kama njia ya kushajiisha uwekezaji wa ndani ya Khilafah na kuepusha uhamishaji wa mali kwenda nje; zifuatazo ni sera tatu ambazo Khaleefah na wasaidizi wake wanaweza kuzitekeleza kivitendo katika uchumi:

**a) Sera ya Kifedha**
Serikali kutoa mikopo isiyo na riba kwa wajasiriamali, kuingia katika ushirika/mudharaba, na kutoa ruzuku, mfano kwa watakao wekeza zaidi katika sekta ambazo uzalishaji wake ni dhaifu au pia maeneo ambayo yana hali ngumu ndani ya Khilafah.

**b) Sera ya Matumizi**
Serikali ielekeze kiwango muwafaka cha matumizi yake katika utafiti na sayansi kupitia kujenga maabara na maktaba za Ummah zitakazo wawezesha kufanya uvumbuzi wa kudumu juu ya miradi kadha wa kadha ya maendeleo ndani ya Khilafah.
**c) Sera ya Kuboresha Miundo Mbinu**
Hii ni kupitia kuimarisha miundo mbinu msingi kama barabara, reli na teknologia ya mawasiliano na mingineyo ili kutia motisha zaidi wajasiriamali katika kuwekeza ndani ya Khilafah.

**Masoud Salim Mazrui**

# Janga la Kiuchumi la Kiulimwengu: Miaka 10 Baadaye

Msimu wa kiangazi wa mwaka wa 2017 ni maadhimisho ya muongo mmoja wa janga la kiuchumi la kiulimwengu. Kampuni ya Lehman Brothers nchini Marekani iliporomoka, masoko ya fedha ya Kiamerika almaarufu kama Wall Street yalianguka na uchumi wa kiulimwengu ukatumbukia katika janga. Trilioni za dola kama mapato zilipotea (dola trilioni 22 za Kiamerika, kwa muda wa miaka mitano), mamilioni ya wafanyikazi waliachwa bila kazi na maelfu ya ahadi zikatolewa na wanasiasa na watunga sera – kila mmoja kuanzia Obama na Gordon Brown mpaka David Cameron na Christine Lagarde – kwamba mambo yatabadilika. Lakini, karibu muongo mmoja baadaye, kinacho shangaza zaidi ni kuwa mabadiliko ni machache. Muongo mmoja huku kukiwa bado kuna kadhia nyingi zilizo sababisha janga hili ambazo hazija tatuliwa, huku wahalifu wake wakipewa uangalizi mzuri na serikali za Kimagharibi kwa kupewa usaidizi wa kifedha (ili kuzuiwa kuporomoka kwa makampuni yao yaliyo feli) na uchapishaji wa pesa.

Uchumi wa nchi kubwa za kiulimwengu unaendelea kujikokota kufikia kudumisha uzalishaji wake, licha ya miaka kadhaa ya kuuamsha kupitia sera za kifedha na matumizi. Uchumi wa nchi nyingi changa pia unakumbwa na changamoto za kimuundo za muda mrefu, zikiwemo deni linalo ongezeka, raia wakongwe, na uhaba au ubovu wa miundo msingi.

Kiasi kikubwa cha pesa duni zilizo tengezwa ziko katika benki kuu ya Amerika ya Federal Reserve, benki kuu ya Uingereza ya Bank of England na benki kuu ya Ulaya ya European Central Bank (ECB) ambazo zimesukumwa na wawekezaji wa kifedha katika masoko yalio na uzalishaji mkubwa ya Afrika Kusini, Brazil na India, miongoni mwa masoko mengine. Wanauchumi katika Bank for International Settlements, ambayo ni benki kuu ya benki kuu, wanaamini kuwa dola trilioni 9.8 za Kiamerika zimetolewa kutoka benki za kigeni kama mikopo na dhamana katika nusu ya kwanza ya muongo huu baada ya Lehman Brothers kuporomoka. Kiasi cha dola trilioni 7 za Kiamerika ya pesa hizo zimelekezwa kwa masoko yanayo ibuka.

Tangu janga hili la kifedha mnamo 2007, msururu wa hatua za dharura zilichukuliwa sio tu kuokoa uchumi wa nchi za kimagharibi bali kuukoa mfumo mzima wa mabenki. Kulikuwa na tishio la kweli la kusambaa kwa uporomokaji wa mabenki kwa sura ya kudorora kwa uchumi ikitabiriwa kuwa kama 1930. Mabenki yaliinuliwa kwa zaidi ya trilioni 21 za Kiamerika ikifuatiwa na msururu wa sera zisizo za 'kawaida' kutoka benki kuu. Yote haya yaliundwa kuiokoa nidhamu, mabenki na kusababisha uzalishaji katika uchumi wa nchi za kimagharibi. Licha ya hatua hizi zilizo husisha pia uchapishaji wa pesa na upunguzaji wa kiwango cha riba kufikia karibu na sufuri, kupona kwa uchumi katika nchi za Magharibi kunakwenda kwa kasi ndogo yenye uchungu mwingi.

Katika mkutano wa kiuchumi wa kiulimwengu wa kila mwaka jijini Davos, Switzerland kuanzia Januari 20 mpaka 23, 2016 viongozi wa kiulimwengu waliamua kuchochea kwa haraka vita vya kifedha ili kuwarahisishia wao kulazimisha uwekaji wa viwango vibaya vya riba. Suluhisho lao kwa 'tatizo' hili mnamo 2016 lilikuwa ni kuusukuma ulimwengu kugeuka kuwa jamii isiyo tumia pesa moja kwa moja katika miamala yake. Mnamo 2016 benki kuu zilianzisha mpangilio huu kupitia kuondoa noti za viwango vikubwa, ambayo inapelekea miamala mikubwa ya kifedha kutoweza kufanyika. Aliyekuwa Seneta wa Amerika Ron Paul alidokeza: "Jamii isiyo tumia pesa moja kwa moja ni ndoto ya IRS: ni kujua na kudhibiti fedha za kila Muamerika." Miongoni mwa matukio muhimu zaidi katika historia ya kiuchumi ya hivi karibuni ni kufichuka kwa stakabadhi milioni 11.5 zinazo onyesha shughuli za kila siku za kampuni ya sheria ya Mossack Fonseca mnamo 2016 ambayo iliyashauri makampuni makubwa ya kiulimwengu, madikteta, wafalme pamoja na viongozi waliochaguliwa kidemokrasia juu ya jinsi ya kuficha pesa zao na kukwepa ushuru.

Tukio hili kwa mara nyengine tena ladhihirisha, kupitia utajiri huu mkubwa wa ushahidi, kuwa huku wengi ulimwenguni wakilazimishwa kwa nguvu kulipa ushuru mkubwa, matajiri na watawala hulipa kiasi kidogo tu kupitia akaunti zao za ng'ambo. Matokeo makubwa ya ufichuzi huu yatakuja pale ufichuzi huu utakapo fichua mabenki na nidhamu ya fedha. Sio siri kuwa utajiri mkubwa umefichwa katika hazina za ng'ambo takwimu zikikadiria kuwa rasilimali zilizofichwa ni asilimia 8 ya utajiri wote wa kifedha wa kiulimwengu ambapo mbeleni hatukuwahi kupata maelezo haya. Na kadhia hii ya utajiri wa ng'ambo ni ishara tu ya saratani kubwa. Pengo kati ya matajiri na masikini umeendelea kukua kwa miongo, na pesa hizi nyingi zilizoko ng'ambo ni ishara ya mtindo huu.

Serikali za kimagharibi zilijiokoa kutokana na mporomoko wa kiuchumi kupitia kuzisaidia kifedha benki zilizo sababisha janga hili. Ufadhili huu ulifanywa kupitia kukata bajeti za serikali na kupunguza ufadhili kwa wasio jiweza katika jamii chini ya kisingizio cha 'sote tumo ndani ya janga hili kwa pamoja'. Waliziba nyufa tu na kuendelea kulingania mfumo wao ulimwengu mzima. Wanaendelea kuwasilisha mfumo wao kama suala nyeti katika kutatua ufukara na deni la kiulimwengu, licha ya kuwa mfumo wao huo huo ndio uliosababisha janga hili la kiuchumi la kiulimwengu.

**Adnan Khan**
**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 4: Nukta ya Maingiliano

Tutazungumzia leo marhala ya pili miongoni mwa marhala za Daa'wah ya Mtume (saw) nayo ni Nukta ya Maingiliano na jamii ili kupatikane: Rai Aam/Rai ya Ummah inayotokana na Waa' yi Aam/Muamko wa Ummah.

Nukta hii ya Pili ilikuwa situ ya maingiliano na jamii bali yalikuwa mapambano yaliyojumuisha mvutano wa kifikra na vitendo vya kisiasa. Mtume (saw) aliifanya Ummul Quraa (Mji Mtukufu wa Makkah) ndio kitovu cha Daa'wah yake na kufika sehemu zilizouzunguka mji wa makkah, baada ya mfumo wa Uislamu kua ndio mwili wa maswahaba wake watukufu, Na zikawa fikra za Uislamu na fahamu zake kwao ndio Njia ya maisha yao.

Maqureysh wakasimama dhidi ya Mtume (saw) msimamo wa Uadui na kutumia mbinu Nne (4) dhidi yake na wafuasi wake.

Tutazitaja katika hii Halaqahna tutazizungumzia kwa ufafanuzi kiasi katika Halaqa Toleo zijazo In Shaa Allah.

1. Ni kumbembeleza/kumrai Mtume (saw) ili awache Da'wah

2. Propaganda/Uvumi dhidi ya Mtume (saw) na  Da'wah.

3. Kuwakata/Kuwatenga Mtume (saw) na Wabebaji Da'wah.

4. Kumuudhi na kumuadhibu Mtume (saw) na Wabebaji Da'wah.

Itaendelea katika UQAB Toleo 9…In Shaa Allah.

# SWALI / JAWABU:
## Natija ya Maridhiano Kati ya Amerika na Ufaransa!



Raisi wa Amerika Donald Trump amerudi tena siku ya Alhamisi kuzungumzia ziara yake ya hivi karibuni nchini Ufaransa. Trump alisema katika mahojiano na gazeti la The New York Times "Ni mtu mkubwa sana", akimkusudia Macron. "Ni mwerevu, mwenye nguvu, anaye penda kunishika mkono wangu." Aliongeza, "Watu hawatambui kuwa anapenda kunishika mkono wangu…" (Al-Arabiya. net-Washington France Press, 20/7/2017). Raisi Trump alizuru Paris mnamo Julai 13, 2017. Raisi wa sasa Macron, alimkaribisha kwa taadhima. Huku raisi wa zamani wa Ufaransa, Hollande, akionyesha kutoridhishwa kwake na raisi huyo wa Amerika, pamoja pia kulikuwa na tuhuma nzito dhidi ya raisi Trump kutoka kwa viongozi wa Ulaya! Maridhiano haya kati ya Amerika na Ufarasa yanaashiria nini na ni yapi malengo ya ziara ya Trump Paris? Na je, kuna natija zozote za ziara hii kwa hali ya Syria, hususan tangu raisi wa Ufaransa Macron kuzungumza kuhusu mkakati mpya wa kifaransa na kiamerika nchini Syria?

**Jibu:** uzembe wa Trump katika siasa za kimataifa umekuwa na matokeo ya kuchukiza, kwa mfano, taarifa zake za kushtua juu ya uwezo wa NATO, zilipelekea majibizano makali dhidi ya sera ya kiamerika, na miongoni mwa majibizano hayo yaliyojitokeza hadharani yalitolewa kutoka Berlin. Wakati wa kampeni yake ya uchaguzi na baada ya kutawazwa kuwa raisi mnamo 20/1/2017, Trump hakuficha kuchukizwa kwake na Muungano wa Ulaya. Aliipongeza kura ya maoni ya Uingereza ya kutaka kujitoa katika Muungano wa Ulaya (Brexit). Balozi wa Amerika Jijini Brussels alitarajia kuvunjika kwa Muungano wa Ulaya, na Amerika ilisubiri kura za Uholanzi na Ufaransa kwa matarajio ya ushindi kwa wanaopinga Muungano wa Ulaya, ili kuvunjika huku kwa Muungano wa Ulaya kutokee mwaka wa 2017. Hili ndilo ambalo Ulaya ilisimama kidete dhidi ya kutokea kwake; ilifaulu katika kuzuia athari ya maandamano ya Kiingereza kwa Uholanzi na Ufaransa, na hivyo basi kuondoa tishio la kuvunjika kwa Muungano wake. Uzembe wake katika siasa za kimataifa ukaongezeka tena kisha akarudi nyuma kutokana na maamuzi yake. Trump aligeuza maoni yake juu ya NATO kama muungano uliopitwa na wakati, kama alivyo usifu, kisha akarudi nyuma juu ya misimamo hii hadharani. Vile vile alijiondoa kutoka katika makubaliano ya Paris kuhusu hali ya anga, na kuagiza majadiliano yake mapya, kisha akasimama katika ukingo wa vita na Korea Kaskazini, na kurudi nyuma baadaye. Zaidi ya hayo, alibeba mtazamo mbaya juu ya China, baadaye akashirikiana nayo huku akisubiri matokeo yake kutoka katika faili ya Korea Kaskazini, akatoa taarifa nzito juu ya eneo la Syria na baadaye akawaachia mambo yake majirani zake wa Astana na Geneva.

Kile ambacho pia chaweza kuonekana ni usumbufu wa hali yake ya ndani hususan upinzani ulioonyeshwa juu ya sera yake katika kadhia ya usaidizi wa Urusi kwake wakati wa uchaguzi. Natija ya matatizo haya na upinzani huu

*Endelea Uk..14*

ni kuwa mawasiliano ya raisi na wanachama wa idara yake kwa Urusi ilikuwa kadhia moto sana nchini Amerika, na hali hii haikumsaidia raisi huyu kufaulu kuunda mkataba baina ya Urusi na Amerika na kwamba ulicheleweshwa, na Trump alifanya mkutano mmoja tu na raisi wa Urusi juu ya ajenda za kongamano la G20 jijini Hamburg, Ujerumani mnamo Julai 7, 2017. Mahusiano baina ya Amerika na Urusi yamezidi kuwa magumu katika wakati ambapo bunge la congress linashinikiza vikwazo vya ziada juu ya Urusi. Hii ikiwa ni ziada ya masaibu ya ongezeko la ripoti za kiamerika juu ya kujiingiza kwa Urusi katika kura za Amerika, hili likiongeza zaidi fedheha kwa raisi ndani ya nchi, bila ya kutaja kuendelea kwa fedheha kupitia kuyarudisha tena mahusiano ya nchi yake na Moscow.

Yote haya yamesababisha kuvurugika kwa siasa ya kimataifa baina ya Amerika na Muungano wa nchi za Ulaya, na kuvurugika huku kumeleta uzuri na ubaya kulingana na maslahi ya nchi hizi na uwezo wao wa kupatiliza hali mpya ya siasa ya kiamerika, tutaiangalia upya misimamo ya nchi hizi kuhusiana na sera ya Trump na kisha kugusia natija ya msimamo wa Ufaransa iliyo pelekea kualikwa kwa Trump kuzuru Paris na kukaribishwa kwa taadhima.

1 – Ama kuhusu Uingereza: ziara ya mapema ya waziri mkuu wa Uingereza Theresa May ya Washington mnamo Januari 20, 2017 na hamu yake ya kutia saini makubaliano ya kibiashara na Washington ni mfano kwa nchi nyengine za Muungano wa Ulaya wa kuzishajiisha kujiondoa katika Muungano huo. Hivyo basi, Uingereza ilirudisha tena mafungamano yake na Amerika na iliipendelea zaidi idara ya Trump, lakini baada ya matarajio ya Amerika ya kuuvunja Muungano wa Ulaya kusambaratika, kama ilivyo shuhudiwa kwa ushindi wa wanaounga mkono muungano huo katika uchaguzi nchini Uholanzi na Ufaransa, mtazamo mzuri aliokuwa nao Trump kwa Uingereza ukabadilika kwani alitaka Uingereza iwe ndio inayoongoza mchakato huo wa kuuvunja Muungano wa Ulaya, na kwa kuwa hali ya kujiondoa London katika Muungano wa Ulaya haikujirudia jijini Paris (Ufaransa) na Amsterdam (Uholanzi), Amerika imerudi tena kuchafua maslahi ya kimataifa ya Uingereza katika hali iliyoishtua London. Amerika inamshinikiza kibaraka wake, Sisi, kuongeza usaidizi wake kwa Hafter (mkuu wa jeshi la Libya) pasi na kutilia maanani maslahi ya Uingereza nchini Libya, na Amerika pia akawasukuma vibaraka wake kutia mshtuko kiasi ili kuishinikiza Qatar, ambayo ni msaada mkubwa kwa Uingereza katika ardhi za kiarabu na kiislamu. Kwa haya na mengineo, sera ya Uingereza ilitingishwa na hivyo kupoteza imani kwa Trump, huku ikijipata katikati ya nyundo ya Amerika upande mmoja, na kinoo cha Ulaya, ambayo ili jadili kuondoka katika muungano wake, kwa upande mwengine. Katika hali ya tashwishi hii pana, waziri mkuu wa Uingereza akatangaza uchaguzi mapema, hili liliwashangaza hata viongozi serikalini, na kwa haya tarehe ya matokeo ya uchaguzi ikapangwa kuwa 8/6/2017, Uingereza ikajikuta kwenye njia panda baina ya kuondoka katika Muungano wa Ulaya au kurudi kwake. Uchaguzi huu ulionyesha kuwa wanaounga mkono kujiondoa katika muungano walizidi kuwa dhaifu, hali iliyo ongeza uwezekano wa kubakia ndani yake ikiwa majadiliano na Brussels (Ubeligiji) hayata zaa makubaliano yanaoiridhisha. Hii inaonyesha jinsi gani siasa mpya ya Amerika ilivyo ichanganya Uingereza.

2 – Katika upande ulio muhimu zaidi ni upande wa Urusi; testuri za Ulaya zililingana na zile za Amerika baada ya eneo la Crimea kuunganishwa na Urusi mnamo 2014 na kuchochea mashariki mwa Ukraine. Vikwazo vya Kiamerika na Ulaya vya ashiria kukubaliana kimaoni baina yao kuhusiana na hofu ya Ulaya inayo tokana na kulengwa kwa eneo la Ulaya mashariki na Putin, lakini tangu wakati wa kampeni yake ya uchaguzi, Trump amekuwa makini na vikwazo hivi na ameapa kujenga mafungamano ya karibu na Urusi jambo lililo ichanganya Ulaya na kuiacha peke yake katika sura ya kuinuka upya kwa Urusi. Licha ya kuwa viongozi wa Ulaya wametambua kuwa Amerika, wakati wa idara ya Obama, ndio iliyo iruhusu Urusi kuinuka, hususan baada ya kujihusisha katika vita vya Syria, Trump alitishia kusonga mbele zaidi kufanya makubaliano ya pamoja na Urusi katika kadhia za kiulimwengu, jambo litakalo yaondoa matarajio ya Ulaya ya kuwa na dori katika migogoro ya kimataifa.

3 – Ama kuhusu Ujerumani, ilichukua hatua za wazi kuikataa siasa mpya ya kiamerika; ilikataa kashfa za kiamerika dhidi ya nchi za Ulaya za NATO, ikapinga kujiondoa kwa Amerika katika makubaliano ya hali ya anga na kukataa kuwepo kwa majadiliano mapya juu yake. Ili kashifu mkataba wa silaha ambao Trump alitia saini na Saudi Arabia na kuuona kama kutia moto ndani ya mafuta katika eneo ambalo tayari lawaka moto, na kubakia na msimamo huu licha ya Ufaransa kubadilisha msimamo wake. Kulingana na matangazo ya jioni ya shirika la habari la Deutsche Welle: ((Misimamo ya chansela wa Ujerumani Angela Merkel ilikuwa mikali kwa raisi wa Amerika wakati wa kikao cha G20 nchini Ujerumani, lakini raisi wa Ufaransa alikuwa makini kutomuudhi Trump…)), (Deutsch Welle, 14/7/2017). Kiujumla, yaweza kusemwa kuwa Ujerumani imeongeza pakubwa majaribio ya kuamka tena kama dola kuu yenye nguvu, yote ni kutokana na kuibuka sera mpya za kiamerika.

4 – Baada ya hayo, tunagusia kuhusu maana ya ziara ya Trump nchini Ufaransa, maridhiano yaliopo sasa katika ya Amerika na Ufaransa, malengo ya Ufaransa ya kumualika raisi Trump kuzuru na kushiriki katika siku ya kitaifa ya Julai 13, 2017, kuangazia kile ambacho Ufaransa anakiita kumbukumbu ya Amerika ya kushiriki katika vita vya kwanza vya dunia, ambayo ni tukio la kale na ambalo ni nadra sana kufanywa

*Endelea Uk..15*

kupitia kwa sherehe isipokuwa kwa lengo maalum. Katika wakati ambapo raisi Trump anavutana kimahusiano na Ulaya nzima, Ufaransa ilimualika kushiriki katika sikukuu yake ya kitaifa! ((Macron katika maongezi ya simu mnamo Jumanne alitoa mualiko mpya kwa Trump kuzuru Ufaransa na kushiriki katika sikukuu yake ya kitaifa. Mualiko wa kwanza ulikuwa wakati wa mkutano wa NATO mwishoni mwa mwezi Mei mwaka jana jijini Brussels…)) (Elaph newsite, 28/6/2017). Katika mkutano wa G20, uliofanyika Ujerumani mnamo 7/7/2017, raisi Macron wa Ufaransa alilegeza kamba kwa unyenyekevu ya kutomtenga Trump miongoni mwa viongozi, hususan wa Ulaya, walioshutumu vikali kujiondoa kwa Amerika katika makubaliano ya hali ya anga. Trump mwenyewe alishangazwa na mualiko wa Macron katika mazingira kama haya. ((Trump alisema "ameshangazwa" kupokea ualishi huu baada ya uamuzi wake wa kujiondoa kutoka kwa makubaliano ya hali ya anga ya Paris, yaliotiwa saini na nchi 195 mnamo 2014…)) (Al Arabiya.net, 20/07/2017)

5 – Ama kuhusu malengo ya muelekeo huu mpya wa Ufaransa, ni lazima isisitizwe kuwa Ufaransa, ambayo ni nguzo muhimu zaidi ya Muungano wa Ulaya, ilikuwa makini kwa Trump na kuhofia natija ya siasa yake juu ya mahusiano kati ya Amerika na Ulaya. Hofu hii haikumsaza pia raisi wa zamani wa Ufaransa Hollande. Raisi wa sasa, Macron, pia amekuwa makini sana kwa Trump tangu kampeni yake ya uchaguzi na mpaka hivi karibuni. Mkengeuko huu wa Ufaransa kwa Amerika umejitokeza tu wiki kadhaa zilizo pita, na umejitokeza wazi wazi kwa ualishi wa raisi wa Amerika Trump kuzuru Ufaransa na kupokewa kwa taadhima na kuzungakwa na heshima kubwa. Udadisi juu ya mkengeuko huu unatoa taswira mbili; na zote ni muhimu:

Taswira ya kwanza ya mkengeuko huo inahusu hali ya Syria. Baada ya Macron kutangaza kuwa: haoni badali halali ya Bashar, na kwamba Ufaransa haioni tena suala la kuondoka Bashar kama sharti la mapatano. (Reuters, Juni 21, 2017). Na akasema baada ya hayo na kabla ya kumpokea raisi wa Amerika: "Tumebadilisha mtazamo wa Ufaransa juu ya Syria ili kufikia suluhisho pana la kisiasa, na hatuweki kuondoka kwa Bashar kama sharti kwa hili…" (Middle East, 13/7/2017), hivyo basi Ufaransa imekuwa karibu sasa na Amerika, inayoshikilia karata ya serikali na makundi mengi ya Syria. Muelekeo huu ni kwa lengo la kuwa na dori nchini Syria ambayo amekuwa na hamu nayo kwa muda sasa. Ufaransa inajua fika kuwa haitaweza kuvuta hata harufu ya dori hiyo bila ya kupata idhini kutoka kwa Amerika.

Kwa hivyo, kukaribisha kwa taadhima na kusisitiza kutoondoka kwa Bashar yote ni kwa sababu Ufaransa inajua kwamba Amerika haitaki kuondoka kwake kwa sasa, isipokuwa baada ya matayarisho ya kupatikana badali ya kibaraka mwengine kuchukua mahali pake, na kwa sasa Amerika bado haijampata. Ufaransa ilianza kubwaga misimamo yake ya mwanzoni kwa sababu ilikuwa ni vizingiti vinavyomzuia yeye kushiriki (katika kadhia ya Syria). Ufaransa ilianza kuimba wimbo wa "vita dhidi ya ugaidi", kwa kufuata mpangilio sambamba na wa Trump. Raisi wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alisema wakati wa mahojiano ya pamoja ya waandishi wa habari na mwenzake wa Amerika Donald Trump: kwamba anakubaliana na raisi Trump juu ya muelekeo wa hali baada ya vita nchini Iraq na Syria. Mnamo Alhamisi katika mji mkuu wa Ufaransa Macron akaongeza kusema kuwa anakubaliana pia na raisi wa Amerika kufanya kila jitihada kupambana na ugaidi… (Russia Today, 13/7/2017).

Taswira ya pili ni hofu ya Ufaransa juu ya kukua kwa dori ya Ujerumani; hofu hii imeifanya Ufaransa kuipinga Ujerumani. Huku tuhuma za Ujerumani dhidi ya Trump zikiongezeka, Ufaransa inajikaribisha zaidi (kwa Trump)! Punde tu baada ya ziara raisi wa Amerika jijini Paris, balozi wa Ufaransa katika Umoja wa Mataifa, Francois Delattre, alisema kuwa: "Kundi la kimawasiliano nchini Syria ambalo Paris inapendekeza kubuniwa, linapaswa kuhusisha wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na washirika wa kieneo. Balozi huyu aliwaambia wanahabari katika kikao cha faragha cha Baraza la Usalama, mnamo Ijumaa jioni, kwamba timu hiyo iliotajwa hapo juu ni lazima itekeleze "uenezaji wa amani na kutayatisha ramani ya muelekeo". Mjumbe huyu wa Ufaransa aliongeza kuwa jambo muhimu zaidi kwa sasa ni kuunganisha jamii ya kimataifa na kuanzisha miradi mipya itakayo saidia jitihada za balozi maalum wa Ufaransa nchini Syria, Stefan de Mistura... (Russia Today, 14/7/2017). Hivyo basi, Ufaransa inatoa wito wa kubuniwa kwa "kundi la kimawasiliano chini Syria lijumuishe nchi wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na washirika wa kieneo" na "kuzalisha mradi imara kwa nchi tano zitakazo jihusisha (na Syria)" yaani kutengwa kwa Ujerumani kutokana na dori hii kwa kule kuwa si mwanachama wa Baraza la Usalama, ni jambo linalo fichua wasiwasi wa Ufaransa juu ya kuinuka kwa Ujerumani; kamwe haitaki iwe na dori ya kimataifa.

6 – Hivyo basi, kuvurugika kwa sera ya Trump, hususan ziara yake nchini Ufaransa, imesababisha mabadiliko katika siasa ya kimataifa baina ya Amerika na Muungano wa Ulaya kiasi cha kuwa baadhi ya vyombo vya habari vinaichukulia ziara hiyo ya raisi wa Amerika Donald Trump jijini Paris, kuwa ndio mwanzo wa mpangilio mpya wa kiulimwengu, ambapo raisi wa Ufaransa Emmanuel Macron anaongoza nchi yake katika mahusiano mapya ya Amerika na Ujerumani. Gazeti lilisema kuwa Macron anajiwasilisha kama kiongozi mwenye akili katika Muungano wa Ulaya baada ya Uingereza kujiondoa kutoka kwa Muungano huo. Karata za Ulaya zitagawanywa baada ya Uingereza kujiondoa, kwa mujibu wa gazeti. Tahariri ya gazeti hili ilitamatisha kwa kusema kuwa Muungano wa Ulaya

Endelea Uk..16

umeundwa katika hali isiyo iwezesha Ujerumani wala Ufaransa kusimama kama dola iliyo na nguvu kipekee na kwamba nchi mbili hizi ziliweza kumaliza uhasama wa makarne baina yazo na hatimaye kufanya kazi pamoja katika kuliongoza Bara Ulaya Uingereza ikiweko au bila ya Uingereza. Lakini kwa sasa zinaogelea katika mawimbi tofauti; Ufaransa iko chini ya uongozi wa Macron, iliyo na ari ya kuongoza Ulaya, na Ujerumani chini ya uongozi wa Merkel, ina angazia namna ya kudumisha Ulaya yenye uwezo kamilifu. (Al-Wafd website, 14/7/2017).

7 – Tunachotaka kutamatisha katika jibu hili ni kuwa ndoto za Ufaransa za kuingia eneo la Syria hazitakuwa za muda mrefu, hatimaye zitagongana na uhakika wa msimamo wa Amerika ambayo inakubali tu kuwepo na usimamizi mmoja juu ya mgogoro wa Syria, na baadhi ya upole ambao Amerika ina uonyesha kwa harakati za kifaransa nchini Syria ni tu kwa ajili ya kuchochea ugomvi kati ya Ufaransa na Ujerumani ndani ya Muungano wa Ulaya ili kuuvunja.

Ama kuhusu hofu ya Ufaransa ya kuinuka kwa Ujerumani, ni hofu ya kihakika; msingi wa muundo wa serikali ya Kijerumani unaupiku msingi wa muundo wa serikali ya Kifaransa. Hili linajulikana kihistoria na kijografia. Katika wakati ambapo kwa sasa Ujerumani kimaadili ina achana na kujifunga na makubaliano ya vita vya pili vya dunia yanayo inyima dori ya athari ya kijeshi ya kiulimwengu, kwa kuyatupilia mbali, ni wazi kuwa itaibuka tena barani Ulaya, ikiwa na nguvu kushinda Ufaransa, hata kama itajikaribisha na Amerika kiasi gani.

Twamuomba Allah (swt) aukoleze zaidi ugomvi kati yao na hatimaye jengo lao liporomoke:

فَأَتَى اللَّهُ بُنْيَانَهُم مِّنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِن فَوْقِهِمْ وَأَتَاهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ

**"… Allah akayang'oa majengo yao kutoka kwenye misingi, dari zikawaporomokea juu yao, na adhabu ikiwajia kutoka wasiko kujua"** [An-Nahl: 26] na serikali ya kiislamu kuchukua mahali pao na kueneza kheri ulimwenguni, na maneno ya Mtume (saw) katika hadith yake yadhihiri. Katika Musnad ya Imam Ahmad kutoka kwa Tamim Ad-Dari ambaye amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah (saw) akisema:«لَيَبْلُغَنَّ هَذَا الْأَمْرُ مَا بَلَغَ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَلَا يَتْرُكُ اللَّهُ بَيْتَ مَدَرٍ وَلَا وَبَرٍ إِلَّا أَدْخَلَهُ اللَّهُ هَذَا الدِّينَ بِعِزِّ عَزِيزٍ أَوْ بِذُلِّ ذَلِيلٍ عِزًّا يُعِزُّ اللَّهُ بِهِ الْإِسْلَامَ وَذُلًّا يُذِلُّ اللَّهُ بِهِ الْكُفْرَ..» **"Hakika jambo hili litafika kila sehemu yenye kufikiwa na usiku na mchana wala Allah hataiwacha nyumba yoyote isipokuwa ataingiza dini hii kwa izza kubwa au udhalilifu mkubwa – kwa izza atayo upa Uislamu na udhalilifu atakao udhalilisha kwayo ukafiri."**

Al-Bayhaqi pia amepokea hadith sawa na hii katika Sunan Al-Kubra vile vile katika Mustadrak ya Hakim. Na hili litapatikana kwa uwezo na usaidizi wa Allah, na hilo sio gumu kwa Allah.

29 Shawwal 1438 H
23/7/2017 M

